
Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

# JARIDA

TOLEO LA MEI, 2021

## UZINDUZI WA BARAZA KUU JIPYA LA 47 LA WAFANYAKAZI WA NSSF MKOANI MOROGORO




## YALIYOMO


*Waziri Jenista aagiza .....* Uk.....01

*Maisha ni hadithi ......* Uk.....03

*4 Kali zilizobamba* Uk.....04


Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

**NSSF**


Simu Bure 0800116773

customercare@nssf.or.tz

www.nssf.or.tz

@NssfTanzania

# WAZIRI JENISTA AAGIZA BARAZA LA WAFANYAKAZI LA NSSF KUWA CHACHU YA UTOAJI HUDUMA BORA KWA WANACHAMA



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mhe. Jenista Mhagama akizungumza na wajumbe wa Baraza la 47 la wafanyakazi wa NSSF*

**Na MWANDISHI WETU**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mhe. Jenista Mhagama, ameliagiza Baraza la 47 la Wafanyakazi wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), kuwa chachu katika kuhakikisha kila mtumishi anatimiza wajibu wake wa kutoa huduma bora kwa wanachama, kuacha uzembe, vitendo vya rushwa na ubabaishaji kazini.

Mhe. Jenista alitoa maagizo hayo mwishoni mwa wiki, wakati akizindua Baraza la 47 la Wafanyakazi wa NSSF, mkoani Morogoro, ambapo aliwahimiza watumishi wa Mfuko huo kuendelea kufanya kazi kwa uweledi na ufanisi ili kuondoa changamoto mbalimbali zinazowakabili wanachama na wadau wao.

Alisema majukumu ya Baraza hilo ni kuchambua mbinu na mikakati mbalimbali inayoibuliwa ili Mfuko upate mafanikio na ufanisi uliokusudiwa, kutafakari na kuishauri Menejimenti mbinu za uandikishaji wanachama na kuongeza kasi katika ukusanyaji michango kutoka sekta binafsi na sekta isiyo rasmi.

Waziri Jenista alisema jukumu lingine la Baraza hilo, ni kupitia na kushauri mikakati ya utoaji wa huduma bora kwa wanachama, wastaafu na wadau wengine wa Mfuko kwani eneo hilo bado lina changamoto kubwa.

Kwa mujibu wa Waziri Jenista, Baraza pia lina jukumu la kushauri mbinu za kuboresha uwekezaji na vitega uchumi katika Mfuko, kwamba hilo ni eneo lingine lenye changamoto kwa kuwa siku za nyuma baadhi ya miradi ya vitega uchumi haikuzingatia weledi katika utekelezaji wake.

# HABARI PICHA

## WAZIRI JENISTA MHAGAMA AKIFUNGUA BARAZA KUU JIPYA LA 47 LA WAFANYAKAZI WA NSSF












# MAISHA NI HADITHI FANYENI KAZI KWA UAMINIFU ASEMA MWENYEKITI WA BODI NSSF

## *Awataka wafanyakazi wa NSSF kuwa wazalendo na waadilifu

**Na MWANDISHI WETU**

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Balozi Ali Iddi Siwa, amewataka wafanyakazi wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), kufanya kazi kwa uzalendo na uweledi wa hali ya juu huku wakilitanguliza Taifa mbele.

Alisema hayo mkoani Morogoro katika uzinduzi wa Baraza jipya la 47 la wafanyakazi wa NSSF, na kusisitiza kuwa maisha ni hadithi hivyo basi wafanyakazi wa NSSF waifanye hadithi ya Mfuko huo iwe nzuri ili baadaye wapate kusimuliwa vyema.

Balozi Siwa aliweka wazi kwamba kufanya kazi kwa uzalendo na bidii kunatoa sehemu kubwa sana ya kutengeneza hadithi nzuri ya Mfuko, hivyo basi wafanyakazi hao wanapaswa kujitoa zaidi kwa maslahi mapana ya Mfuko, jamii na Taifa kwa ujumla.

“Kazi ni sehemu kubwa sana ya maisha yetu, kwa hiyo kazi ina nafasi kubwa ya kutengeneza hadithi yetu, kazi ina mchango mkubwa kwenye kutengeneza hii hadithi ya maisha,” alisema Balozi Siwa.



*Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Balozi Ali Iddi Siwa akizungumza na wajumbe wa Baraza Kuu la 47 la wafanyakazi wa NSSF*



# 4 KALI ZILIZOBAMBA



**Balozi Ali Iddi Siwa**
*Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya NSSF*

*Kazi ni sehemu kubwa sana ya maisha yetu, kwa hiyo kazi ina nafasi kubwa ya kutengeneza hadithi yetu, kazi ina mchango mkubwa kwenye kutengeneza hii hadithi ya maisha. Kwa hiyo ninachotaka kuwaomba tuitumie kazi ili iwe hadithi kubwa sana tunayojaribu kuitengeneza.*



**Amina Chayowa**
*Mwakilishi wa NSSF Mkoa wa Morogoro.*

*Tutahakikisha tunaifikia sekta isiyo rasmi kwani ina watu wengi, ili tuweze kuongeza mapato kwenye Mfuko, pia tutafanya kazi kwa bidii ili tuweze kupata wanachama wengi watakaochangia NSSF.*



**Aloyce Thomas**
*Mjumbe Kurugenzi ya Ukaguzi wa Ndani.*

*Naamini mengi yamebebwa na yataenda kufanyiwa kazi kwa maana ya kutazama maslahi ya wafanyakazi, lakini pia kuwatazama wanachama namna gani ambavyo stahiki zao wanapatiwa kwa namna sheria inavyozungumza.*



**Katonga Jaffari**
*Mwakilishi wa NSSF Mkoa wa Geita.*

*Kazi kubwa ya Mfuko kwa sasa ni kuhakikisha kwamba tunatoa huduma bora kwa wanachama wetu, hivyo katika utoaji wa huduma kwa wanachama wetu lazima tuangalie vitu gani ambavyo vitatusaidia kutoa huduma bora na moja wapo ni lazima tuendane na mifumo bora na ya kisasa katika utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku.*

# MKURUGENZI MKUU WA NSSF ATAJA VIPAUMBELE MUHIMU KUTATUA KERO ZA WANACHAMA



*Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa NSSF, Masha Mshomba akizungumza na wajumbe wa Baraza Kuu la Wafanyakazi NSSF*

**Na MWANDISHI WETU**

Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba, amemuhakikishia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mhe. Jenista Mhagama, kuwa katika mpango na bajeti ya Mfuko ya mwaka ujao wa fedha yaani 2021/2022, wamejikita zaidi katika kuondoa kero mbalimbali hasa za wanachama.

Mshomba alisema katika kufanikisha hilo watahakikisha wanaandikisha wanachama kutoka sekta binafsi na sekta isiyo rasmi.

Alisema wataboresha huduma kwani kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wanachama, hivyo wameelekeza nguvu katika kulitekeleza hilo.

Mshomba alisema wanatarajia kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa Mfuko huo ili waweze kuelewa taratibu za NSSF.

Alisema pia watatoa mafunzo kwa wafanyakazi watoa huduma kwa wanachama ili waweze kuvaa viatu vya wanachama kwa kuzingatia maadili ya Mfuko.

Kwa mujibu wa Mshomba, watajenga timu moja kwani bila ya kuwa na timu moja katika Mfuko mkubwa kama NSSF wanaweza wasifikie malengo, hivyo watawafanya wafanyakazi kuwa sehemu ya Mfuko huo.

Mkurugenzi Mkuu huyo wa NSSF alisema wataweka mazingira bora ya kazi kwakuwa ni jambo muhimu na kwamba amemuomba Waziri Jenista kuwaunga mkono.

Alisema wamejielekeza kwenye suala zima la usimamizi madhubuti hasa kwa Menejimenti na Bodi kwamba katika kutoa huduma bora lazima usimamizi uwe madhubuti ili waweze kufanikiwa katika malengo yao.

# TUMEJENGEWA MISINGI IMARA
# WASEMA WAJUMBE WA BARAZA LA WAFANYAKAZI LA NSSF



**Na MWANDISHI WETU**

Baadhi ya wajumbe wa Baraza la 47 la Wafanyakazi wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) wamesema kikao cha baraza hilo kimewajengea misingi imara ya kwenda kutoa huduma bora kwa wanachama na wadau wa Mfuko huo.

Akizungumza katika mahojiano maalumu mara baada ya kufungwa kwa kikao hicho, Mwakilishi wa NSSF Mkoa wa Morogoro, Amina Chayowa, alisema kazi kubwa iliyo mbele yao ni kwenda kutoa huduma bora kwa wanachama na kwamba watahakikisha changamoto zote zinazowakabili wanachama na wadau zinapatiwa ufumbuzi.

Naye, Aloyce Thomas ambaye ni mjumbe kutoka Kurugenzi ya Ukaguzi wa Ndani, alisema yote waliyojadiliana katika kikao hicho yataenda kufanyiwa kazi hasa katika kutatua changamoto za wanachama.

Kwa upande wake, Katonga Jaffari, Mwakilishi wa NSSF Mkoa wa Geita, alisema kazi kubwa ya Mfuko kwa sasa ni kuhakikisha kwamba unatoa huduma bora kwa wanachama wake.

"…katika utoaji wa huduma kwa wanachama wetu lazima tuangalie vitu gani ambavyo vitafikia tutoe huduma bora moja wapo ni lazima tuendane na mifumo bora na ya kisasa katika utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku," alisema Jaffari.



## *Hatua muhimu za kuchukua unapostaafu*

1. ***Wasilisha*** *nyaraka zako muhimu ofisi yoyote ya NSSF.*
2. ***Kamilisha*** *taratibu zote za kufungua madai.*
3. ***Subiri*** *malipo yako ndani ya mwezi mmoja.*

Tunajenga Maisha Yako
ya Sasa na Baadaye

Tunajenga Maisha Yako
ya Sasa na Baadaye

NSSF